



**TANZANIA ARTISTS RIGHTS ORGANIZATION (TARO)**  
**(TAASISI YA HAKI ZA WASANII)**

S.L.P 70624 Dar es salaam, Simu:+255785769223,+255767292581  
Barua pepe:tarotanzania@gmail.com,Mitandao ya kijamii:instagram/fb, taro.tz  
Anwani ya Ofisi: Mtaa wa Kihonzile , Mkabala na Daraja la kuelekea Bagamoyo,  
Kata ya Mabwepande , Wilaya ya Kinondoni, Mkoa wa Dar es Salaam

“Tunasimama kwa ajili ya Haki na Maslahi ya wasanii wote”

Kumb na: Taro /P/2022/ A15

**: Swahili Version:**

Tarehe: 30 Mei 2022

**PONGEZI KWA BASATA KWA KUMTAMBUA NA KUMUENZI JUDITH PETER**  
**NGUSA (MISS UNITED NATIONS 2022).**

Rejea kichwa cha habari hapo juu. **Tanzania Artists Rights Organization (TARO)** au kwa lugha ya Kiswahili “**TAASISI YA HAKI ZA WASANII**” ni shirika lisilo la kiserikali lililosajiliwa kushughulikia haki na maslahi ya wasanii wote Tanzania.

Tarehe 28 Mwezi Februari 2022, kupitia andiko letu lenye kumbukumbu namba **Taro /P/2022/ A06**, TARO tuliandika taarifa kwa umma kuwataka **BASATA** kuwaenzi na kuwatambua wasanii wenye uwezo na vipaji maalumu bila **UBAGUZI**. Tuliwarejea wasanii wachache ambao hawakutambuliwa na kuenziwa na **BASATA** kwa kazi nzuri za sanaa walizofanya kuhusiana na Utamaduni wa nchi yetu kwenye soko la kimataifa, ikiwajumuisha **Lutengano Mwakisopile** (Mshindi wa Tuzo Ya Kimataifa Ya Ubunifu Ya Oscar (OSCAR OF AFRICAN CREATIVITY-2019), **Kili Paul** na **Neema Paul** (Walitambuliwa na Waziri Mkuu wa India, Mheshimiwa Narendra Modi kupitia mtandao wa Tweeter (wenye wafuasi milioni 76.3) kwa kazi kubwa ya sanaa ya uchekeaji kwa kuchanganya tamaduni za kimasai na kihindi.

Mnamo tarehe 12 Mwezi Mei 2022, **Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA)** kupitia mtandao wake wa instagram iliweka taarifa inayomhusu **Judith Peter Ngusa** (Mshindi wa mashindano ya urembo ya Umoja wa mataifa 2022/Miss United Nations 2022), ambapo walimuenzi na kumpongeza kwa ushindi aliouleta nchini. (**kama inavyoelekeza Sera Ya Utamaduni-1998**)

Kwa jambo hilo, tunalipongeza sana **Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA)** kupitia **Kaimu Mtendaji wake (Bw. Matiko Mniko)** kwa kupokea na kufanyia kazi maoni yetu yenye lengo la kuiboresha sanaa yetu nchini. *Taro tunalipokea jambo hili kwa furaha sana kama moja ya mafanikio ya kazi zetu.* Tutaendelea kutoa maoni yetu pale panapohitaji kukoselewa au kuelimisha na tutapongeza pale panapohitaji kupongeza, huku tukizingatia, heshima ya utu, haki za binadamu na utawala wa sheria. Pia tutatoa ushauri wa kitaalam pale panapohitaji ushauri.

**ASANTENI**

(Kazi iendelee)

**Wako katika kujenga Taifa**

**Mkurugenzi Mkuu wa Utawala**  
**WAKILI JOSHUA MSAMBILA**